# Ascension Wisconsin
# Taarifa ya Pamoja ya Mbinu za Faragha

TAARIFA HII INAELEZEA JINSI MAELEZO YAKO YA MATIBABU YANAVYOWEZA KUTUMIKA NA KUTOLEWA NA JINSI UNAVYOWEZA KUFIKIA MAELEZO HAYA. TAFADHALI ISOME KWA MAKINI.

**Ahadi Yetu**
Tumejitolea kudumisha faragha na usiri wa maelezo yako ya afya. Taarifa hii inakufahamisha kuhusu haki zako kuhusiana na maelezo yako ya afya na jinsi tunavyoweza kutumia na kutoa (kutuma) maelezo yako. Tunalinda pia usiri wa rekodi zako za ugonjwa wa matumizi ya dawa za kulevya kulingana na sheria ya kitaifa inayoitwa Part 2 (Sehemu ya 2), katika vituo vinavyotoa huduma za mipango ya Part 2 inavyoelezwa katika taarifa hii.

**Nani Anayefuata Taarifa Hii**
Taarifa hii inafuatwa na wafanyakazi wote, wafanyakazi wa huduma ya matibabu, wakurufunzi, wanafunzi, watu wa kujitolea, wakandarasi, watoa huduma, maajenti na wafanyakazi wa vituo vya Ascension Wisconsin, kama vile mahospitali, vituo vya matibabu ya wagonjwa wasiolazwa, maduka ya dawa, maabara na vituo vya shughuli za matibabu. Vituo vingine vinaweza kutenda kama Shirika Mshirika Linalolindwa (Affiliated Covered Entity) kwa makusudi ya utiifu wa Kanuni za Sheria ya Uwajibikaji na Uhamishaji wa Bima ya Afya (Health Insurance Portability and Accountability Act, HIPAA). Ascension Wisconsin pia inashiriki katika Mpangilio wa Kikundi cha Huduma za Afya (Organized Healthcare Arrangement) na vituo vingine vya Ascension vinavyoweza kutumia na kutumiana maelezo yako ya matibabu, malipo na shughuli za huduma za afya zinazohusiana na mipangilio hii na inavyoruhusiwa na Kanuni za HIPAA. Ili ufahamu orodha kamili ya vituo hivi, tafadhali wasiliana na Afisa wa Faragha wa Ascension Wisconsin ("Afisa wa Faragha") inavyoelezwa katika taarifa hii.

**Jinsi Tunavyoweza Kutumia na Kutoa Maelezo Yako**
Taarifa hii inaelezea njia tunazoweza kutumia na kutoa maelezo yako ya afya na tunapohitaji ruhusa yako ya maandishi kufanya hivyo. Tunaweza kuwasiliana nawe kwa simu, barua pepe au ujumbe wa maandishi kwa namba au anwani unayotupatia. Kawaida tutatumia njia zilizosimbwa kwa njia fiche kuwasiliana nawe kielektroniki, lakini mawasiliano mengine yanaweza kutumwa bila kusimbwa kwa njia fiche, kama vile ujumbe wa maandishi, na ukitupatia namba yako ya simu au barua pepe unakubali kupokea ujumbe kwa njia hiyo.

Mara nyingi tunatumia na kutoa maelezo yako kwa makusudi ya matibabu, malipo na shughuli za afya. Kwa mfano, hii inamaanisha tunaweza kutumia na kutoa maelezo yako:

- ili kukupa huduma za afya, na watoa huduma wengine wa afya wanaokutibu, au na duka la dawa kwa kujaza dawa zako za kuagizwa na daktari.
- na kampuni ya bima yako au mlipaji mwingine kudai malipo ya huduma au kupata idhini ya kutoa huduma au dawa.
- kuendeleza biashara yetu, kuboresha huduma, kuelimisha wataalamu wetu na kutathmini utendaji wa mtoa huduma.
- na washirika wetu wa biashara, wanaotoa huduma kwa au kwa niaba yetu, kama vile huduma ya malipo, wanaotusaidia katika shughuli zetu za biashara. Washirika wetu wote wa biashara wanahitajika pia chini ya Kanuni za HIPAA kulinda faragha na usalama wa maelezo yako ya afya.
- kutayarisha kikundi kidogo cha data au maelezo yasiyomtambulisha mtu. Kikundi kidogo cha data huondoa vitambulisho vingi na tukiituma kwa mtu mwingine yeyote anaweza tu kuitumia kwa makusudi fulani yanayoruhusiwa na Kanuni za HIPAA na lazima atie saini makubaliano yanayomtaka alinde maelezo hayo. Baada ya maelezo ya afya kuondolewa kabisa maelezo yanayomtambulisha mtu, kanuni za ulinzi wa faragha zilizo katika Taarifa hii hazitumiki tena, na yanaweza kutumika kwa makusudi yoyote ya kisheria, ikijumuisha kubuni vipimo, taratibu au bidhaa mpya za biashara.

Tunaweza kutumia zana za akiliunde ("Artificial Intelligence, AI") kwa makusudi yaliyoelezwa hapo juu na katika Taarifa hii na inavyoruhusiwa na Kanuni za HIPAA na sheria nyingine zinazotumika. Kwa mfano, tunaweza kutumia zana zinazorekodi mawasiliano yako na watoa huduma na wafanyakazi wetu ili kusaidia kutayarisha madokezo au kupanga miadi. Watoa huduma wetu wakati mwingine wanaweza kutumia zana za AI,

ikijumuisha kwa makusudi ya utambuzi wa ugonjwa, ili kukusaidia kukupa matibabu bora, lakini zana hizi hazichukui nafasi ya uamuzi wa watoa huduma hawa. Tunaweza pia kutumia zana za AI kusaidia katika shughuli zetu, kama vile kutayarisha mawasilisho ya kielimu, kupanga wafanyakazi wetu, na takwimu za hospitali kama vile ukaguzi wa muda wa kukaa hospitalini.

Tunaweza pia kutumia au kutoa maelezo yako ya afya kuwasiliana nawe kwa sababu zifuatazo:

- kukuambia kuhusu chaguo nyingine za matibabu zinazoweza kupatikana, huduma mpya, fursa za kushiriki katika utafiti, fursa za kutupatia maoni kuhusu huduma zetu na manufaa au huduma nyingine zinazohusiana na afya.
- kukuambia kuhusu matibabu yako na huduma zijazo ikijumuisha miadi, vikumbusho vya kujaza upya dawa au ujumbe kama huo kuhusu matibabu yako.
- kwa makusudi ya kuchangisha pesa ya Ascension. Unaweza kuamua kukataa kutumiwa ujumbe huu kwa kujibu kama inavyosema kwenye ujumbe au kwa kuwasiliana na Afisa wa Faragha.

Tunaruhusiwa pia, na wakati mwingine sheria inatutaka, tutumie au tutoe maelezo yako kwa wapokeaji fulani. Tunaweza kutakiwa tutimize masharti fulani kabla tuweze kutumia au kutoa maelezo yako kwa makusudi haya. Baadhi ya mifano inajumuisha:

- Afya na usalama wa umma: kuripoti magonjwa ya kuambukiza, watoto waliozaliwa au watu waliofariki; kuripoti vitendo vya dhuluma, kupuuzwa au vurugu za nyumbani; kuripoti athari mbaya ya dawa; kuepuka hatari kubwa ya kiafya au kiusalama (maelezo ya Part 2 yataondolewa maelezo yanayomtambulisha mtu kabla ya kutolewa)
- Utekelezaji wa sheria: kutambua au kumpata mshukiwa, mtoro au mtu aliyepotea; kuripoti tukio la uhalifu kituoni
- Kesi za mahakama na kiusimamizi: kujibu amri ya mahakama au ya kiusimamizi, kama vile wito wa kufika mahakamani
- Malipo ya wafanyakazi na maombi mengine ya serikali: kesi au madai ya malipo ya wafanyakazi; mashirika ya usimamizi wa afya kwa shughuli zilizoidhinishwa kisheria; kazi maalum za serikali (shughuli za kijeshi, usalama wa kitaifa)
- Msaada wa janga: kuonyesha eneo uliko na hali ya jumla kwa makusudi ya kufahamisha familia au marafiki zako na mashirika yaliyoidhinishwa kisheria kusaidia katika hali za dharura
- Kutii sheria: kwa Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ili kuona kama tunatii sheria ya faragha ya kitaifa
- Utafiti: kujitayarisha kwa utafiti; kuchambua rekodi kama sehemu ya mradi ulioidhinishwa na Bodi ya Ukaguzi wa Mashirika (Institutional Review Board, IRB) na hazina hatari kubwa kwa faragha yako; tafiti zinazohusisha tu maelezo ya watu waliokufa
- Kuambatana na matumizi au ufichuzi unaoruhusiwa: kuita jina lako katika eneo la kusubiri kwa sababu ya kuhudhuria miadi na wengine wanaweza kusikia jina lako likiitwa. Tunajitahidi tuwezavyo kupunguza matumizi au ufichuzi huu unaombatana
- Kwa msimamizi wa mazishi, afisa mchunguzi wa vifo au mchunguzi wa matibabu inavyohitajika kufanya kazi zao
- Kwa mashirika yanayoshughulikia uchangaji wa viungo, tishu au macho na ubadilishaji wa viungo inavyohitajika kufanya kazi zao

Tunashiriki pia katika ubadilishanaji wa maelezo ya afya, au (Health Information Exchanges, HIE), kwa utoaji wa maelezo yako kielektroniki kwa sababu ya matibabu yako na makusudi mengine yanayoruhusiwa na Kanuni za HIPAA au yanayohitajika kisheria. Washiriki wengine wa HIE wanatakiwa pia kulinda maelezo yako. Unaweza kuzuia maelezo yako yasipatikane katika HIE kwa makusudi yote yasiyohitajika kisheria kwa kuwasiliana na Afisa wa Faragha inavyoelezwa katika Taarifa hii.

Katika hali zifuatazo, tunaweza kutumia au kutoa maelezo yako isipokuwa ukataze au ukitukataza hasa. Kama huwezi kutupatia ruhusa yako, kwa mfano ukiwa umepoteza fahamu, tunaweza kutoa maelezo yako tukiona kuwa ni kwa faida yako.

- Kwa familia, marafiki au wengine wanaohusika katika matibabu au malipo ya matibabu yako. Kwa mfano, tunaweza kuambia familia yako unavyoendelea baada ya upasuaji.
- Kwa saraka ya kituo na huduma za ukasisi.

Katika hali zifuatazo, tutatumia au kutoa tu maelezo yako ya afya ukitupatia ruhusa yako ya maandishi. Unaweza kuondoa ruhusa hii wakati wowote (isipokuwa kwa kiwango ambacho tumeitumia) kwa kuwasiliana na Afisa wa Faragha.

- kwa makusudi ya utangazaji (inavyoelezwa na Kanuni za HIPAA).
- kwa uuzaji wa maelezo yako au kwa malipo kutoka kwa watu wengine.
- kwa utoaji fulani wa maelezo ya tiba ya saikolojia.
- kwa sababu nyingine yoyote ambayo haijaelezewa katika Taarifa hii.

Utumiaji na utoaji wetu wa maelezo fulani nyeti unaweza pia kuzuiwa zaidi na sheria nyingine za kitaifa au za jimbo, ikiwa ni pamoja na lakini sio tu kwa maelezo ya Part 2 inavyoelezwa katika sehemu ya Rekodi za Part 2 katika Taarifa hii. Hii inajumuisha maelezo yanayohusiana na matumizi ya pombe na dawa za kulevya, jenetiki, afya ya akili na Virusi vya Ukosefu wa Kinga Mwilini/Ukosefu wa Kinga Mwilini (Human Immunodeficiency Virus, HIV/Acquired Immunodeficiency Syndrome, AIDS).

Unapaswa kufahamu kwamba ikiwa maelezo yako yametolewa kisheria, kwa ombi lako au kwa njia iliyoelezwa hapo juu kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo, yanaweza kutolewa upya na yasilindwe tena kulingana na sheria ya kitaifa na ya jimbo.

**Haki Zako**

Kuhusiana na maelezo yako ya afya, una haki fulani. Unaweza kutumia haki hizi ilivyoelezwa katika Taarifa hii au kwa kuwasiliana na Afisa wa Faragha. Maombi mengine yanatakiwa kutumwa kwa maandishi. Unaweza:

- **Kufikia, kukagua na kunakili maelezo** tunayotumia kufanya maamuzi kuhusu matibabu yako. Una haki ya kukagua na kupewa nakala ya karatasi au ya kielektroniki. Ukiomba nakala ya maelezo, tunaweza kukutoza ada inayofaa. Tutakupa nakala au muhtasari ndani ya siku 30 (au mapema kulingana na sheria ya jimbo) na kukufahamisha kuhusu ucheleweshaji wowote au ikiwa hatuwezi kutimiza ombi lako.
- **Kuomba mawasiliano ya siri.** Unaweza kutuomba tuwasiliane nawe kwa njia fulani. Tutasema "ndiyo" kwa maombi yote yanayofaa na tutajibu ndani ya siku 60.
- **Kuomba kuzuiwa.** Unaweza kutuomba tupunguze maelezo tunayotumia au kutoa kwa sababu ya matibabu, malipo na shughuli za afya. Si lazima tukubali ombi lako na tunaweza kusema "hapana". Unapolipia huduma mwenyewe, kikamilifu, na utuombe tusitoe maelezo hayo kwa mtoa huduma wa bima yako, tutasema "ndiyo" isipokuwa tutakiwe kutoa maelezo hayo kisheria. Tutakufahamisha ndani ya siku 30.
- **Kuomba kurekebishwa.** Unaweza kutuomba turekebishe (kubadilisha) maelezo yako ya afya ikiwa si sahihi au hayajakamilika. Tunaweza kusema "hapana" kwa ombi lako, lakini tutakuambia sababu kwa maandishi ndani ya siku 60 au kukufahamisha ikiwa tunahitaji muda zaidi, lakini si zaidi ya siku 30 za ziada.
- **Kupewa orodha ya tuliowatumia maelezo yako.** Unaweza kuomba orodha (rekodi) ya mara tulizotoa maelezo yako na sababu miaka sita nyuma, au miaka mitatu kwa rekodi za Part 2, kutoka tarehe ya kutuma ombi lako. Si mara zote za ufichuzi (utumaji) wa maelezo zitakazojumuishwa katika orodha hii, kama vile maelezo yaliyotolewa kwa sababu ya matibabu, malipo, au shughuli za huduma za afya, isipokuwa kwa rekodi za Part 2 zilizotolewa kupitia rekodi ya afya ya kielektroniki. Tutakupa rekodi moja bila kukulipisha ndani ya siku 60 au kukufahamisha kama tunahitaji muda zaidi, lakini si zaidi ya siku 30 za ziada, lakini tunaweza kukutoza ada ya gharama inayofaa ukiomba rekodi nyingine ndani ya miezi 12.
- **Kupata nakala ya Taarifa hii.** Unaweza kutuomba tukupatie nakala (karatasi au ya kielektroniki) ya Taarifa hii wakati wowote au kuangalia nakala kwenye tovuti yetu katika https://healthcare.ascension.org/npp.
- **Kuchagua mtu wa kukuwakilisha.** Ikiwa umempa mtu mamlaka ya kukuwakilisha kwa matibabu au ikiwa mtu ni mlezi wako wa kisheria, mtu huyo anaweza kutumia haki zako na kufanya maamuzi kuhusu maelezo yako ya afya. Wakati mwingine, mtoto mdogo anaweza kufanya maamuzi au kutumia haki zake mwenyewe.
- **Kuwasilisha malalamiko.** Unaweza kuwasilisha malalamiko ikiwa unahisi haki zako zimekiukwa. Unaweza kuwasiliana na Afisa wa Faragha au Ofisi ya Haki za Kiraia ya Idara ya Afya na Huduma za Binadamu ya Marekani (U.S. Department of Health and Human Services Office for Civil Rights) inavyoelezwa katika Taarifa hii. Hutaadhibiwa, kubaguliwa, kulipizwa kisasi au kutishwa kwa kuwasilisha malalamiko.

**Majukumu Yetu**

- Tunatakiwa kisheria kudumisha usiri na usalama wa maelezo yako ya afya.
- Tutakufahamisha ikiwa tukio la ukiukaji litatokea ambalo linaweza kuwa limeathiri usiri au usalama wa maelezo yako ya afya yanayokutambulisha.
- Lazima tufuate mbinu zilizolezewa katika Taarifa hii. Tuna haki ya kubadilisha masharti ya Taarifa hii na mabadiliko hayo yatatumika kwenye maelezo yako yote tuliyonayo. Tutakupatia nakala ya Taarifa hii katika https://healthcare.ascension.org/npp.
- Hatutatumia au kutoa maelezo yako, ikijumuisha maelezo yako ya Part 2, kando na inavyoelezwa hapa isipokuwa uturuhusu kwa maandishi. Ukituruhusu, unaweza kubadilisha mawazo yako wakati wowote. Tufahamishe kwa maandishi kama utabadilisha mawazo yako.

**Maswali au Malalamiko na Jinsi ya Kutumia Haki Zako**

Ikiwa una swali au ungependa kutumia haki zako zilizoelezwa katika Taarifa hii, tafadhali wasiliana na Afisa wa Faragha wa Ascension Wisconsin aliyeko 400 W. River Woods Parkway, Glendale, WI 53212, kwa simu kwa nambari 877-565-4896, au kwa barua pepe katika compliance.wisconsin@ascension.org. Maombi mengine ya kutumia haki zako yanatakiwa kutumwa kwa maandishi. Ili kuwasilisha malalamiko kwa Ofisi ya Haki za Kiraia, tuma barua kwa 200 Independence Avenue, SW, Washington, DC 20201, piga simu kwa nambari 877-696-6775, au tembelea www.hhs.gov/ocr/privacy/hipaa/complaints/.

**Rekodi za Part 2**

Kuongezea kwa kanuni za ulinzi wa faragha za Kanuni za HIPAA na haki zilizotolewa inavyoelezwa katika Taarifa hii, usiri wa rekodi za ugonjwa wa matumizi ya dawa kulevya unalindwa na sheria nyingine ya kitaifa inayoitwa Part 2. Vituo fulani vya Ascension hutoa huduma za mipango ya Part 2, na sehemu hii inawapa wagonjwa wanaoshiriki katika mipango hiyo maelezo ya ziada kuhusu sheria na kanuni zinazosimamia rekodi hizo.

Kanuni za ziada za ulinzi zifuatazo zinatumika kwa matumizi na utoaji wa maelezo yako ya Part 2 na zinaelezea haki zako.

- Tunaweza kukuomba utie saini idhini moja ya matumizi yote ya baadaye au utoaji wa maelezo yako ya Part 2 kwa makusudi ya matibabu, malipo na shughuli za afya. Tukitoa rekodi za Part 2 kwa idhini yako, maelezo hayo yanaweza kutolewa tena na mpokeaji bila ruhusa yako kadri inavyoruhusiwa na Kanuni za HIPAA.
- Hatutatumia au kutoa maelezo yako ya Part 2 kwa makusudi ya kuchangisha pesa isipokuwa tuwe kwanza tumekupa fursa ya kuchagua kukataa kupokea mawasiliano ya kuchangisha pesa.
- Hatutatumia au kutoa rekodi za Part 2 kwa kesi yoyote ya kiraia, uhalifu, kiusimamizi au kisheria inayokuhusu, isipokuwa tupate ruhusa yako ya maandishi au amri ya mahakama. Tunaweza tu kutoa rekodi hizo kulingana na amri ya mahakama baada ya wewe na sisi kupokea notisi na kupewa fursa ya kusikilizwa. Amri ya mahakama inayoidhinisha utumiaji au utoaji wa rekodi hizo lazima pia iwe na wito wa kufika mahakamani au masharti mengine ya kisheria yanayohitaji kutolewa kwa rekodi hizo kabla ya rekodi hizo kutumiwa au kutolewa.
- Maelezo ya Part 2 yataondolewa maelezo ya kumtambulisha mtu kabla ya kutolewa kwa makusudi ya afya ya umma tusipopata ruhusa yako.
- Tunaweza kuomba ruhusa yako ya maandishi kwa matumizi na utoaji wa maelezo ya Part 2, ikiwa ni pamoja na lakini sio tu kutoa maelezo ya Part 2: kwa sajili kuu au kwa usimamizi wa shughuli za uondoaji ili kuzuia kuandikishwa mara nyingi; kwa mtu katika mfumo wa utekelezaji wa haki ya uhalifu na ikiwa kushiriki katika mpango wa Part 2 kunahitajika ili kufungwa kwa kesi ya uhalifu; kwa mpango wa jimbo wa uchunguzi wa dawa zinazoagizwa na daktari ikiwa inahitajika na sheria ya jimbo.
- Unaweza kuondoa idhini yoyote kwa kuwasiliana na mpango wa Part 2 au Afisa wa Faragha.
- Una haki ya kujadili Taarifa hii na Afisa wa Faragha.
- Unaweza kuomba orodha (rekodi) ya mara tulizotoa maelezo yako ya Part 2 na sababu kwa hadi miaka mitatu nyuma kabla ya tarehe ya kutuma ombi lako. Maelezo yaliyotolewa kwa sababu ya matibabu, malipo au shughuli za huduma za afya yatajumuishwa tu ikiwa yalitumwa kupitia rekodi ya afya ya kielektroniki.
- Unaweza kuomba orodha ya mara ambazo maelezo yametolewa na mtu au shirika lililopokea maelezo kwa idhini yako ya maandishi kwa hadi miaka mitatu nyuma kabla ya tarehe ya kutuma ombi lako na watatoa orodha ya watu ambao rekodi zao zimetolewa. Utapokea jibu ndani ya siku 30 au chini yake.

- Kama tumekubali ombi lako la kuzuia utumiaji au utoaji wa maelezo yako ya Part 2 kwa makusudi ya matibabu, tunaruhusiwa na bado tunaweza kutoa maelezo hayo kwa watoa huduma wengine wa afya katika hali ya matibabu ya dharura, lakini tutaomba mtoa huduma huyo wa afya asitumie au kutoa zaidi maelezo hayo.

Taarifa hii itaanza kutumika kutoka tarehe 1/1/2026.